

TANZANIA BREWERIES PUBLIC LIMITED COMPANY

MKUTANO MKUU WA 49 WA WANAHISA

**KUMBUKUMBU ZA MKUTANO KATI YA WANAHISA WENYE HISYA CHACHE NA
WAWAKILISHI WAO KATIKA BODI ULIOFANYIKA KATIKA UKUMBI WA
MIKUMI – JNICC TAREHE 25 AGOSTI 2022 KUANZIA SAA 3.00 ASUBUHI**

WALIOHUDHURIA

BI. V. MORDICHAI : Mwakilishi - Mwenyekiti wa Mkutano
BW. M. CHANDE : Mwakilishi
WAJUMBE WENGINE : Wameorodhesha katika mahudhurio ya Mkutano Mkuu

WENGINE WALIOHUDHURIA

HURUMA NTAHENNA : Katibu

WAALIKWA

BW. L. MUSUSA : Mwenyekiti wa Bodi
BW. J. MORAN : Mkurugenzi Mtendaji
BW. E. BUSARA : Mwezeshaji Semina kwa Wanahisa

KUMB. 1/2022 : KUFUNGUA MKUTANO

1.1.Mkutano Mkuu wa Wanahisa ultanguliwa na Mkutano kati ya Wawakilishi wa wenyehisa chini ya asilimia 8 kila mmoja amba ni Bw. Maharage Chande na Bibi Violet Mordichao waliochaguliwa katika Mkutano Mkuu wa 48.

1.2.Baada ya uchaguzi, ilikubaliwa kuwa Mkutano Mkuu wa Wanahisa utanguliwe na Mkutano kati ya Wanahisa wenyehisa chache pamoja na wawakilishi wao. Lengo ni kutoa taarifa ya utendaji hadi kipindi cha mkutano na fursa kwa Wanahisa kujadiliana, kupata ufanuzi na kutoa ushauri kwa Wawakilishi kadri watakavyoona inafaa.

KUMB. 2/2022 : TAARIFA YA UTENDAJI JANUARI -JUNI 2022

2.1.Wawakilishi walitoa taarifa ya utendaji wa Kampuni kwa kipindi cha miezi sita ya Mwaka 2022 yaani kuanzia tarehe 1 Januari 2022 hadi tarehe 30 Juni 2022. Katika kipindi hicho, Kampuni ilifanya vizuri na kufanikiwa kuongeza mauzo ikilinganishwa na Mwaka uliopita. Mapato ya Kampuni yaliongezeka kwa asilimia 13, kutokana na ongezeko kubwa la mauzo ya bia na ongezeko la wastani la mauzo ya vinywaji vikali. Hii ililitokana na Kampuni kuwa na bidhaa mbalimbali zinazopendwa na kutawala soko.

2.2.Faida ya uendeshaji iliongezeka kwa asilimia 26 ikichangiwa na ongezeko la mauzo na ufanisi katika kusimamia gharama za uendeshaji. Gharama za usafirishaji na usambazaji ziliongezeka kwa asilimia 19 kutokana na athari za mfumuko wa bei na kupanda kwa bei ya mafuta. Pia kulikuwa na ongezeko la gharama za uendeshaji na usimamizi kutokana na ongezeko la gharama za vipuri lililosababishwa na mabadiliko ya sera ya uhasibu. Hata hivyo, gharama za mauzo na masoko zilipungua katika kipindi hicho kutokana na kusitishwa kwa mpango wa promosheni za mauzo sambamba na kupunguzwa kwa promosheni za bidhaa ikilinganishwa na kipindi kama hicho mwaka uliotangulia.

2.3.Kutokana na ongezeko la mauzo na kupungua kwa gharama za uendeshaji, kiwango cha faida ya uendeshaji kiliongezeka kwa asilimia 2 na kufikia asilimia 18.4 ikilinganishwa na asilimia 16.4 ya Mwaka jana. Faida ya kampuni baada ya kulipa kodi kwa kipindi hicho ilikua kwa asilimia 10 ikilinganishwa na mwaka uliopita kutokana na ongezeko la mauzo. Fedha zilizotokana na uendeshaji zilikuwa shilingi milioni 125,868, ambapo kati ya fedha hizo shilingi milioni 34,466 zilitumika kulipa kodi ya mapato, shilingi milioni 24,271 zilitumika katika kuboresha viwanda, na shilingi milioni 4,491 kutumika katika kulpia masuala mbalimbali na pesa zilizobaki zilihifadhiwa kwa ajili kwa kufanikisha mipango ya baadaye ya ukuzaji biashara.

KUMB. 3/2022 : SEMINA YA UWEKEZAJI

3.1.Mwenyekit alimkaribisha Bw. Emilian Busara ambaye aliendesha mafunzo kuhusu fursa na changamoto za kuwekeza kwenye hisa. Wanahisa walipata fursa ya kuuliza maswali kuhusu mada iliyowasilishwa na masuala mengine kuhusiana na uwekezaji na mwezeshaji aliyajibu ipasavyo.

KUMB. 4/2022 : MAJADLILIANO

4.1.Wajumbe waliwashukuru wakurugenzi kwa uwasilishaji mzuri wa taarifa za utendaji na walitaka ufanuzi juu ya mikakati ya kuhimili ushindani na kuhakikisha kunakuwa na ukuaji endelevu. Katika kujibu suala hilo, Mkurugenzi Mtendaji aliwafahamisha Wanahisa kuwa hilo litafanikiwa kwa kuendelea kuongoza katika ubunifu. Akitoa mfano, alisema hivi karibuni

Kampuni ilizindua chapa tatu mpya za bidhaa katika soko na itaendelea kuwa kinara wa ubunifu ili kuendelea kutawala soko.

- 4.2.Wajumbe waliishukuru Menejimenti na Wawakilishi kwa kuandaa mafunzo ya uwekezaji katika hisa na walipendekeza jambo hilo liendelee katika mikutano ijayo. Wanahisa walipendekeza kuwa, katika siku zijazo, TBL ifikirie kuandaa chakula cha mchana au chakula cha jioni baada ya mkutano mkuu ili kutoa fursa ya kufanya majadiliano zaidi kati ya wajumbe, bodi na viongozi wa kampuni.
- 4.3.Wanahisa wenye changamoto au wanaohitaji ufanuzi kuhusu gawuio walishauriwa kuonana na Katibu wa Kampuni na kuthibitisha taarifa zao kwa kuwa gawio la hisa hulipwa moja kwa moja benki na si kwa hundi kama ilivyokuwa katika.

KUMBU. NA. 5/2022 : KUFUNGA MKUTANO

- 5.1.Wawakilishi waliwashukuru Wanahisa kwa mahudhurio na michango mizuri na kuwatakiia Mkutano Mkuu mwema na wenye tija. Mutano ulifungwa saa 09hrs55.

ZIMETHIBITISHWA :-----
MWENYEKITI

TAREHE :-----